**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA ANUAI NA. 263 YA MWAKA 2023**

**KESI KUMBUKUMBU (REFERENCE) NA. 20230920000528020**

**KITENGE SHOMVI ............................................................ MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF**
**CHAMA CHA MAPINDUZI ................................ MJIBU MAOMBI WA KWANZA**
**UMOJA WA WAZAZI TANZANIA ............................ MJIBU MAOMBI WA PILI**
**REGISTERED TRUSTEES OF**
**UMOJA WA WAZAZI ............................................. MJIBU MAOMBI WA TATU**
**KATIBU MKUU UMOJA WA WAZAZI ....................... MJIBU MAOMBI WA NNE**

# MAAMUZI

**Tarehe ya amri ya mwisho**: *28/05/2024*
**Tarehe ya maamuzi:** *31/05/2024*

**MLYAMBINA, J**

Ni madai ya Mleta Maombi kuwa aliajiriwa na Mjibu Maombi kwa nafasi ya Mwalimu wa shule ya Sekondari Tabata hadi tarehe 10/07/2013 alipostaafu. Na baada ya kuona mwajiri wake hatekelezi majukumu yote ya kumlipa stahiki zake aliamua kwenda Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (itajulikana kama Tume) Kanda ya Dar es Salaam na kufungua *Shauri Na. CMA/DSM/KIN/R.928/17/60.* Baada ya kusikilizwa pande zote mbili, tarehe 02/04/2019 Tume ilitoa Tuzo iliyompa ushindi Mleta Maombi kwamba alipwe jumla ya Shilingi 149,526,412/=.

Kwamba, baada ya Tuzo hiyo kutolewa, Mleta Maombi alifungua *Shauri la Kukazia Hukumu Na. 254/2019.* Shauri hilo lilipelekea kwa kufunguliwa kwa maombi mbalimbali ambayo kutokana na kutokuwa na umuhimu katika kesi hii, Mahakama haitayaelezea. Kimsingi maombi mbele ya Mahakama hii yametokana na *Shauri la Kukazia Hukumu Na. 254 la mwaka 2019.* Katika shauri hilo, Mahakama iiiiondoa mali iliyokuwa imewekwa kwa ajili ya kukazia hukumu kwasababu mali hiyo haikuwa ya Wajibu Maombi bali ni ya mtu mwingine ambaye hausiki katika shauri hilo. Pamoja na kuliondoa shauri hilo, Mahakama ilimpa kibali Mleta Maombi kufungua upya kesi yake ya ukaziaji hukumu.

Mleta maombi hakurishishwa na maamuzi tajwa hapo juu, hivyo alifungua mashauri mengine mbaiimbali yatakayoelezewa katika maamuzi haya. Hivyo, basi Mleta Maombi anaiomba Mahakama amri zifuatazo:

i. Kwamba, Mahakama Kuu imuongezee muda kwa ajili ya kuleta maombi ya mapitio ya shauri (Review) kwenye *Maombi ya Kukazia Hukumu Na 254/2019* yaliyotolewa Uamuzi tarehe 19/12/2022 na Naibu Msajili E.M. Kassian.

ii. Kwamba, Mahakama Kuu inaweza kusikiliza na kuongeza muda kwa mamlaka yake kama itakavyoona inafaa.

iii. Kwamba, Mahakama Kuu inaweza kutoa Nafuu yoyote itakayoona inafaa.

Katika kuendesha shauri hili, Mleta Maombi aliwakilishwa na ndugu Hemedi Ombari Kimwaga, Mwakilishi binafsi, ilihali, wakili Fabiani Donatus, aliwawakilisha Wajibu Maombi.

Katika shauri hili Mleta Maombi anaiomba Mahakama kutatua hoja kuu moja:

*Endapo Mleta Maombi ana sababu za msingi za kuchelewa tangu uamuzi wa Maombi ya Kukazia Hukumu Namba 254/2029 ulipotolewa tarehe 19/12/2022.*

Mleta Maombi alieleza kuwa amechelewa kufungua maombi haya kwakuwa alikuwa katika viunga vya Mahakama hii akishughulikia mashauri mbalimbali yanayohusiana na shauri hili. Hivyo aliiomba Mahakama izingatie mashauri hayo na kuruhusu maombi haya. Sababu zake zilipingwa vikali na Mjibu Maombi ambaye kupitia wakili wake alieleza kuwa, Mleta Maombi hakuwa makini kwani aliwasilisha maombi yasiyofaa yaani marejeo badala ya mapitio, hivyo kupelekea mashauri hayo kuondolewa na kusababisha kupoteza muda wa kufungua shauri hili. Ilielezwa kuwa Mleta Maombi hajaeleza sababu za msingi kwanini amechelewa, hivyo basi, shauri lake litupiliwe mbali.

Mahakama imepitia maelezo ya pande zote mbili na kumbukumbu zinaonesha kuwa baada ya maamuzi ya Naibu Msajili kutolewa tarehe 19/12/2022, Mleta Maombi alifungua *Maombi ya Anuai Na. 531 ya mwaka 2022.* Maombi hayo yaliondolewa na Mahakama mnamo tarehe 31/03/2023 kwakuwa yalikuwa na mapungufu kwamba Mleta Maombi aliwasilisha maombi ya anuai badala ya maombi ya marejeo. Baada ya shauri hilo kuondolewa, Mleta Maombi alifungua maombi megine ambayo ni *Maombi Madogo Na. 105 ya mwaka 2023*, maombi hayo pia yaliondolewa tarehe 08/09/2023 kwasababu yalikuwa na mapungufu. Baada ya maombi hayo kuondolewa, mnamo tarehe 11/09/2023, ndipo Mleta Maombi alipowasilisha shauri hili mbele ya Mahakama mnamo tarehe 20/09/2023.

Hivyo basi, kwa mtiririko huo hapo juu, ni wazi kuwa muda mwingi Mleta Maombi alikuwa Mahakamani akiendelea na mashauri mengine yanayohusiana na kesi hii kama alivyowasilisha. Mahakama imezingatia mawasilisho ya Wakili wa Wajibu Maombi kuwa Mleta Maombi alikuwa akiwasilisha maombi ambayo si sahihi. Ni kweli katika kumbukumbu zinaonesha alikuwa akiwasilisha maombi ambayo si sahihi, lakini ni wazi kuwa mkanganyiko huo umeletwa na maamuzi kinzani ya namna ya kupinga maamuzi ya Msajili. Mpaka sasa mkinzano huo haujapatiwa utatuzi, hivyo ni rahisi kwa Mleta Maombi kujichanganya katika kutafuta njia sahihi ya

kupinga maamuzi ya Msajili. Hiyo inaonesha kuwa Mleta Maombi hakukaa tu bali alikuwa akihangaika kushughulikia haki yake. Juhudi kama hizo pia zilijadiliwa katika kesi ya **Mary Mbelle v. Akiba Commercial Bank Ltd,** Miscellaneous Labour Application No. 68 of 2020, High Court, Dar es Salaam ambapo Mahakama iliamua ifuatavyo:

> Under the circumstance of this case, I am of the view that, the Applicant was not reluctant or she did not sleep of her right in pursuing her case. From the date of the impugned decision to date, she showed fully concern about her case. The Applicant has shown diligence and has also accounted for the delay. She has been knocking the doors of this court to be availed with the chance to file the Notice of Appeal. Such efforts cannot be ignored by this Court as they constitute sufficient and reasonable cause to grant an extension of time to file Notice of Appeal.

Pia katika shauri hili, Mahakama haiwezi kupuuzia juhudi alizokuwa anafanya Mleta Maombi kutafuta haki yake ya kusikilizwa. Hivyo basi maombi haya yanakubaliwa. Mleta Maombi anapewa nyongeza ya muda wa siku kumi na nne tokea tarehe ya leo kuweza kuleta shauri lake la mapitio ya maamuzi ya Msajili dhidi ya *Maombi ya Kukazia Hukumu Namba 254/2019.*

Imeamuriwa hivyo.

Y. J. MLYAMBINA

**JAJI**

31/05/2024

Uamuzi huu umesomwa na kutolewa leo tarehe 31/05/2024 mbele ya Mleta Maombi, Hemedi Omary Mwakilishi Binafsi wa Mleta Maombi na bila uwepo wa Wajibu Maombi.

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
(The High Court of Tanzania)
(Labour Division)
DIVISHENI YA MAHAKAMA YA KAZI

Y. J. MLYAMBINA

**JAJI**

31/05/2024